

mavuno ya badaye. Kuvuna wakati wa kiangazi huleta maji maji mengi zaidi na yenye ubora zaidi.

Chipukizi za kando pia huvunwa na kutumika katika kuandaa nasari.

Kuandaa (Utoaji maji maji)

Majani yaliyovunwa hupangwa kwa mviriringo ndani ya beseni ili kuwezesha maji kutoka bila kufinyiliwa.

Maji maji yanaweza kuuzwa katika hali yake asili au yatiwe katika pipa. Kisha yanatiwa motoni taratibu kwa muda wa masaa kumi na mawili. Matokeo basi humwagwa kwenye gunia za kilo 90, ambapo itakaukia ikisha poa, iwe nzito. Kisha huhifadhiwa mahali pasipo na maji tayari kuuzwa au kutumiwa kama kifaa cha urembo au dawa ya kienyeji.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P.57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishi:

Mulindo, J. C na Mukonyi K.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Centre Director,

KARI-Perkerra, S.L.P. 32, MARIGAT,

Simu: (054) 51257

Nukulishi: (054) 30378

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 15 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Kuza Aloe kwa manufaa ya uchumi, afya, na pia kurejesha ubora wa ardhi



Utangulizi

Kuna zaidi ya aina 22 za *Aloe* nchini Kenya lakini aina iliyo maarufu zaidi ni *Aloe vera* ambayo ililetwa nchini kutoka Saudi Arabia na Umarekani.

Mmea wa *Aloe* huwa na majani nyororo na hutoa maji maji ambayo yana manufaa kadha wa kadha.

Aloe ni mmea mwafaka sana katika kuhifadhi mmomonyoko wa udongo na unaweza kupandwa kwenye ardhi zilizo tupu katika sehemu kame na zile kame wastani ili kurejesha ubora na kuzilinda.

Mahitaji ya Ukuzaji

Hali ya anga

Hali iwe kavu na yenye joto kiasi hadi joto jingi.

Mvua

Milimita 300 hadi 700 kwa mwaka lakini udongo mkavu huhitaji kunyunyiziwa mwanzoni ili mimea ikite.

Udongo

Uwe wenye mbolea wastani na unaopitisha maji kwa kiasi (kando ya mlima hufaa zaidi) kwa sababu mmea wenywe huweka maji mengi na unaweza kuugua maji yakizidi.

Asidi ya pH inayofaa ni kati ya sita na saba lakini hustahimili pH ya juu zaidi na pia kiwango cha juu cha virutubishi mseto vya chumvi ya sodium (Na) na ya potassium (K).

Kuzalisha

Aloe huzalishwa kwa kutumia mimea himia-chipukizi na mimea-chipukizi. Upandaji wa mbegu kwenye vitalu vya kupandia vyenye changarawe unawezekana kwa aina zile za kiasili ambazo hutoa mbegu lakini mbinu hii inachosha na huwa na gharama za juu.


Mahitaji ya kitalu

Mifuko ya plastiki hujazwa mchanganyiko wa mchanga, mbolea ya kemikali na mchanga wa ujenzi katika viwango vya 1:2:3.

Michipuko yenye afya na nguvu hutolewa kutoka kwa mti wa mazao na kuwekwa kwenye karatasi za nailoni. Miche hii huwekwa kwenye kitalu ili kuota mizizi na huchukua muda wa miezi miwili.

Matayarisho ya shamba

Aloe hustahimili viwango vikali vya joto lakini ni muhimu kuanza kwa shamba lilolimwa vizuri.



Miche ya aloe katika mifuko ya plastiki

Katika maeneo yalioathirika zaidi, ni sehemu tu za kupandia zinazostahili kuchimbwa.



Shamba lililotayarishwa vema kupandia Aloe

Kupanda

Chimba mitaro mita moja mraba na mashimo umbali wa mita moja ili upate jumla ya miche 5,000 kwa kila ekari.

Mbolea ya shambani ya kipimo cha tani 10 kwa kila ekari itumiwe iwapo mchanga hauna rotuba ya kutosha na irudiwe hiyo baada ya mwaka. Mbolea ya NPK kilo 20 kwa ekari iongezwe kama mbolea ya kawaida.

Utunzaji wa shamba

Wadudu

Mdudu aina ya kindungata huathiri mmea huu lakini hunyunyiziwa dawa iliyochanganywa na mafuta meupe ya kugandisha.

Magonjwa

Ugonjwa wa madoadoa huathiri mmea huu na huangamizwa kwa dawa za kuvu.



Mimea ya Aloe vera

Uvunaji

Majani yaliyokomaa hukatwa na huku ukiacha majani manne machanga kwa kila mmea kwa